HABARI KITAIFA

ZIARA

## Waziri Sangu awatembelea viongozi wa BAKWATA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Kazi, Ajira na Uhusiano, Deus Sangu ametembelea Ofisi za Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Makao Makuu jijini Dar es Salaam na kukutana na viongozi kwa lengo la kujitambulisha na kulitambulisha jukumu jipya la uhusiano ambalo ofisi yake imekabidhiwa kuliratibu.

Alipowasili ofisini huko juzi, Waziri Sangu alipokelewa na Mufti na Mwenyekiti wa BAKWATA, Shekhe Abubakar Zubeir bin Ally pamoja na wajumbe wa baraza hilo.

Akizungumza katika kikao hicho, Waziri Sangu alipongeza baraza hilo kwa mchango wake mkubwa katika kuimarisha amani, umoja na mshikamano nchini.

Alieleza kuwa BAK-

KIBANO

# LATRA yatangaza kibano kwa wamiliki wa mabasi

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imetangaza msimamo mkali kwa mwaka huu, ikisema haitowavumilia wamiliki wa mabasi wanaotumia wahudumu ambao hawajasajiliwa na madereva ambao hawajathibitishwa na mamlaka hiyo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Dk. Habibu Suluo, alisema kuanzia sasa ni wahudumu waliosajiliwa pekee pamoja na madereva waliothibitishwa ndio watakaoruhusiwa kufanya kazi kwenye mabasi ya abiria yanayotoa huduma za usafiri wa mikoani.

"Vinginevyo, tukikukuta mwaka huu unatumia mhudumu ambaye hajasajiliwa au dereva ambaye hajathibitishwa na LATRA, hatutakuvumilia," alisema Dk. Suluo.

Alisema mamlaka hiyo imejipanga kikamilifu kuimarisha usimamizi wa sekta ya usafiri wa mabasi, akisisitiza hakuna mtoa huduma atakayeruhusiwa kukiuka masharti na taratibu zilizowekwa kisheria.

"Tumejipanga kuhakikisha mwaka huu tunazidisha usimamizi ili usafiri wa mabasi uwe salama na wa kuaminika. Ni madereva waliothibitishwa wenye vyeti halali na wahudumu wenye vitambulisho vya LATRA pekee ndio watakaofanya kazi," alieleza.

Dk. Suluo aliongeza kuwa hatua hiyo inalenga kuhakikisha uwajibikaji wa moja kwa moja kwa mhusika anayefanya kosa, badala ya kuadhibu watu wasiohusika.

"Tunahitaji kila mtu awajibike kwa makosa yake. Kama ni kosa la mhudumu, adhabu ichukuliwe dhidi ya mhudumu. Kama ni la dereva, iwe hivyo.

"Ndiyo maana mwaka huu hatutovumiliana, kila mmoja awajibike ili sekta hii iwe salama," alisema.

Vilevile, alisema LATRA itaendelea kushirikiana kwa karibu na Jeshi la Polisi katika kuimarisha usalama wa usafiri wa mabasi, hususan katika kudhibiti ukiukwaji sheria na kulinda usalama wa abiria.

Kwa mujibu wa LATRA, Kanuni ya 17 ya Kanuni za Uthibitishaji Madereva na Usajili wa Wahudumu wa Magari ya Biashara za mwaka 2020, inamtaka mtu yeyote anayekusudia kufanya kazi ya uhudumu katika gari linalotoa huduma za usafiri wa kibiashara kusajiliwa na mamlaka hiyo.

Vilevile, Kanuni ya 20(10) ya Kanuni hizo, chini ya Tangazo la Serikali Na. 81 la mwaka 2020, inamtaka mhudumu aliyesajiliwa kuhakikisha, pamoja na mambo mengine, kuwa gari la abiria halibebi mizigo hatarishi wala kubeba abiria zaidi ya idadi iliyoainishwa kwenye kadi ya gari.

Mhudumu pia anatakiwa kuvaa sare safi na nadhifu kama itakavyoelekezwa na LATRA, kuwa na kadi halali ya usajili na kuwafahamisha abiria masuala yote ya usalama kabla ya safari kuanza na wakati wa safari.

Kanuni hizo zinaelekeza pia kuhakikisha vifaa vya kuhifadhia taka vinakuwamo ndani ya basi na vinatumika ipasavyo, usafi wa ndani ya basi unazingatiwa wakati wote wa safari na abiria wanapatiwa tiketi za kielektroniki ama kwa karatasi au kupitia simu za mkononi.

Kwa mujibu wa LATRA, mhudumu anatakiwa kutoa huduma bora kwa abiria bila kutumia lugha chafu, kashfa au matusi, kuweka alama za utambulisho kwenye mizigo ya abiria na kuhakikisha mizigo hiyo inahifadhiwa sehemu salama.

Pia anatakiwa kuhakikisha burudani inayotolewa ndani ya basi ipo katika kiwango cha chini cha sauti na inazingatia maadili na utamaduni wa Kitanzania.

Kanuni hizo zinakataza mtu yeyote kufanya biashara, kuhubiri, kushiriki shughuli za kisiasa au kutoa burudani zisizoruhusiwa ndani ya basi wakati wa safari.

Kwa msimamo huo, LATRA imesisitiza kuwa lengo lake ni kuimarisha nidhamu, uwajibikaji na usalama katika usafiri wa mabasi, huku ikiwataka wamiliki wa vyombo vya usafiri, madereva na wahudumu wote kufuata sheria ili kulinda maisha ya abiria na kuboresha huduma za usafiri nchini.